



**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**MINISTRY OF ENERGY**  
**ENERGY AND WATER UTILITIES**  
**REGULATORY AUTHORITY**  
**(EWURA)**



**PUBLIC NOTICE**

**A CALL FOR STAKEHOLDERS' VIEWS ON THE MULTI-YEAR TARIFF APPLICATION  
SUBMITTED BY MAKONDE WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY  
(MAKONDE WSSA)**

On 4<sup>th</sup> April 2023, EWURA received an application from Makonde WSSA requesting for approval of multiyear tariffs and fees applicable to water supply services in financial years 2023/24, 2024/25 and 2025/26. Tables 1 to 3 present tariffs, fees, and charges proposed by Makonde WSSA.

**Table 1: Current and Proposed Metered Water Tariffs (TZS/m<sup>3</sup>)**

Customer Category	Current Tariff	Proposed Tariffs		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Domestic	1,400	2,941	4,032	4,044
Institutional	1,500	3,151	4,320	4,333
Commercial	1,600	3,361	4,608	4,622
Industry	1,900	3,991	5,472	5,489
Bulk Water	-	2,101	2,880	2,889
Water Bowser	5,000	10,503	14,400	14,444
Kiosk	1,000	2,101	2,880	2,889
<b>Average Tariff</b>	<b>1,306</b>	<b>2,778</b>	<b>3,809</b>	<b>3,821</b>

**Table 2: Current and Proposed New Connection Fee (TZS/Connection)**

Customer Category	Current Fees	Proposed Fees		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Domestic	20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019	20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019		
Institutional				
Commercial				
Industrial				

**Table 4: Current and Proposed Reconnection Fees (TZS/Reconnection)**

Customer Category	Current Fees	Proposed Fees		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
All customers	50,000	50,000	50,000	50,000

Makonde WSSA explained that the proposed tariff adjustment will enable the utility to implement activities set out in her business plan for the period from 2023/24 to 2025/2026 in order to bring sustainability to water services delivery. Specifically, proposed tariffs and fees will facilitate the utility to recover operational and maintenance costs as well as meet some rehabilitation, replacement and new investment costs hence the provision of adequate, clean and safe water to Makonde WSSA service area, replacing dilapidated water infrastructure, extending the water network, replacement of working tools and other useful assets, increase customer base and population directly served with water.

This public notice is made pursuant to Section 19(4) of the EWURA Act, Cap 414, which requires the Authority to issue a notice of inquiry to collect views from stakeholders including the Government Consultative Council (GCC), Consumer Consultative Council (CCC), Makonde WSSA's customers and the general public on the reasonableness of the proposed tariffs, fees and charges. As part of the inquiry, there shall be a public hearing meeting on Thursday, 18<sup>th</sup> May 2023 at **Newala District Council Hall** in Newala Township from 10:00hrs.

Stakeholders are requested to submit written comments to the Director General through the above-mentioned address at any time by 22<sup>nd</sup> May 2023. More details of the application can be obtained from EWURA Head Quarters located at **EWURA House, 3EWURA Street, 41104 Tambukareli, PO BOX 2857 DODOMA** or **EWURA Eastern Zone Offices, 4<sup>th</sup> Floor, PSSSF Tower, SAM NUJOMA Road, DAR ES SALAAM.**

**Issued by:  
Director General  
EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MAKONDE**

Mnamo tarehe 4 Aprili 2023, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za huduma za maji safi na usafi wa mazingira kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde kwa mwaka 2023/24, 2024/25 na 2025/26. Majedwali namba 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde.

**Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinzazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

Customer Category	Bei za sasa	Bei Zinzazopendekezwa na Makonde		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	1,400	2,941	4,032	4,044
Tasisi	1,500	3,151	4,320	4,333
Biashara	1,600	3,361	4,608	4,622
Viwanda	1,900	3,991	5,472	5,489
Maji kwa Jumla	-	2,101	2,880	2,889
Boza	5,000	10,503	14,400	14,444
Magati	1,000	2,101	2,880	2,889
<b>Wastani wa Bei</b>	<b>1,306</b>	<b>2,778</b>	<b>3,809</b>	<b>3,821</b>

**Jedwali Na. 2: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishwa na Huduma ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)**

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa 2022/23	Ada zinzazopendekezwa		
		2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Sehemu ya 26 ya Kanuni za Maji 2019	Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Sehemu ya 26 ya Kanuni za Maji 2019		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				

**Jedwali Na. 3: Ada za Sasa na Zinzazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi kwa kila Unganisho)**

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinzazopendekezwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Wateja Wote	50,000	50,000	50,000	50,000

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde imeeleza kuwa bei zilizopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kutekeleza kazi zilizoanishwa katika mpango wake wa biashara kwa kipindi cha 2023/24 hadi 2025/26 na hivyo kuwezesha utoaji huduma endelevu ya maji. Mamlaka imebainisha kuwa bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka ya Maji Makonde kugharamia gharama za uendeshaji na matengenezo, ukarabati, ubadilishaji wa miundombinu chakavu na kutekeleza shughuli za uwekezaji mpya ikiwa ni pamoja na kufikisha huduma ya maji katika maeneo mapya, kuongeza wateja na kuongeza kiwango cha wananchi wanaofikiwa na huduma ya maji.

Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA Sura ya 414, kinachoitaka EWURA kutoa tangazo la taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadai ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC), Baraza Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde na Umma kwa ujumla kuhusu bei zinazopendekezwa. Kama sehemu ya taftishi, kutakuwa na mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau utakaofanyika siku ya Alhamisi, tarehe 18 Mei 2023 katika **Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala** uliopo mjini Newala kuanzia saa 4:00 asubuhi.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 22 Mei 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde yanaweza kupatikana kwenye ofisi za **Makao Makuu ya EWURA** zinazopatika katika **Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli, SLP 2857 Dodoma** au **Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki** zilizopo **Ghorofa ya Nne, Jengo la PSSSF, Barabara ya SAM NUJOMA, DAR ES SALAAM.**

**Imetolewa na:  
Mkurugenzi Mkuu  
EWURA**